



ASb
approved

Upepo Mkali

Ursula Nafula

Marion Drew

Kiswahili





Nilikuwa nikicheza na tiara yangu. Upepo mkali ulianza kuvuma.



Upepo huo uliibandua tiara yangu. Ilirushwa mbali.



Macho yangu yalijaa mchanga.



Upepo uligeuka ukawa dhoruba.



Niliogopa!



Nilijiuliza, "Tiara yangu nzuri iko wapi?"



Labda, ilikuwa hewani.



Dhoruba hiyo ilinizungusha. Iliniina juu.



Niliangushwa chini.



Niliposimama, sikuiona tiarayangu. Sikuusikia upepo ukivuma tena.



Nilianza kwenda nyumbani.



Je, unafhamu kuwa upepo mkali ni hatari?

You are free to download, copy, translate or adapt this story
and use the illustrations as long as you attribute in the
following way: Ursula Nafula Author - Ursula Nafula

Adaptation - Ursula Nafula

Illustration - Marion Drew

Language - Kiswahili

Level - First words © African Storybook Initiative 2015

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

